Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania

# TANGAZO LA KUTAFUTA WAKALA WA KUSAMBAZA NA KUUZA VYUNGU (CRUCIBLES) VYA KUYEYUSHIA SAMPULI ZA MADINI YA DHAHABU

Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Madini na ilianzishwa kupitia Sheria ya Madini Sura Na. 123. Jukumu la msingi la GST ni kufanya tafiti za jiolojia ili kubaini aina za miamba na rasilimali madini zinazopatikana nchini kwa lengo la kuchochea uwekezaji hasa katika Sekta ya Madini. Aidha, Taasisi inatoa huduma nyingine ikiwemo huduma za maabara kwa uchunguzi wa sampuli za miamba, udongo na madini.

Mnano mwaka 2020, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia GST ilitenga fedha na kufanikisha ununuzi wa mashine ya kisasa kwa ajili ya kuzalisha vyungu (crucibles) vya kuyeyushia sampuli za madini ya dhahabu wakati wa uchunguzi wa sampuli hizo katika maabara zinazofanya uchunguzi wa madini kwa njia ya tanuru (*fire assay*).

Vyungu hivyo pamoja na kuwa na ubora wa hali ya juu pia vina sifa zifuatazo:-

- Vinahimili tojo la hali ya juu ( hadi nyuzi joto 1400C);
- Vinaweza kutumika tena kwa zaidi ya mara mbili;
- Vina ujazo wa aina mbili (D50 na D55); na
- Vinapatikana kwa bei nafuu.

**Masharti ya kuwa wakala/msambazaji ni kama ifuatavyo:-**

i) Awe na namba ya mlipa kodi na leseni ya biashara;
ii) Awe na eneo/ofisi ya kudumu ya kufanyia hiyo biashara;
iii) Awe na angalau gari moja (1) la kusambazia mzigo
iv) Awe na mtaji wa kununua angalau vyungu elfu kumi 10000 kwa mara moja;
v) Awe mzoefu wa usambazaji bidhaa za uchimbaji madini na uchunguzi wa sampuli kwenye maabara za madini.
vi) Awe tayari kuelimishwa na GST juu ya masuala ya usambazaji na uuzaji wa vyungu hivyo;

GST katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kuuza crucibles husika kupitia mawakala. Hivyo, mawakala wenye nia ya kusambaza na kuuza crucibles husika wanaalikwa kutuma maombi yao yakiwa katika nakala ngumu na laini kwa Mtendaji Mkuu, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) **S.L.P 903 Dodoma**, Barua pepe: **madini.do@gst.go.tz,** Simu **+255262323020**. Waombaji wanatakiwa kuambatisha kwenye barua zao za maombi nakala ya leseni ya biashara, TIN, Tax Clearance, Bank Statement ya miaka miwili kuanzia 2023. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 09/05/2025.